

Wasifu wa Mkurugenzi Mkuu Dkt. Agnes Lawrence Kijazi

Dkt. Agnes Lawrence Kijazi ni Mkurugenzi Mkuu wa TMA ambaye aliteuliwa rasmi tarehe 11 Septemba 2011 hivyo kutakiwa kuwa mwakilishi wa kudumu WMO kutoka Tanzania

Dkt. Agnes Lawrence Kijazi ni mjumbe wa kamati kuu ya WMO na ataitumikia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2015 hadi 2019.

Kabla ya kuwa Mkurugenzi Mkuu Dkt. Kijazi ameitumikia TMA kwa kipindi cha miaka 27 akiwa kwenye ngazi ya afisa na baadae Uongozi, vilevile amekuwa mfano wa kuingwa katika uwakilishi wa nchi kwenye shughuli mbalimbali za kimataifa ikiwa ni sambamba na kushika nyadhifa za juu kwenye kamati za Kikanda, Afrika na Ulimwenguni.

Dkt. Kijazi mwenye Shahada ya uzamivu (PhD) katika masuala ya hali ya hewa kutoka Chuo Kikuu cha Cape town, Afrika Kusini na akiwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi ya uongozi wa juu TMA ameweza kuifikisha TMA katika mafanikio makubwa yakiwemo:

- ✓ kuiwezesha nchi kupata cheti cha Kimataifa katika utoaji huduma za hali ya hewa kwenye sekta ya usafiri wa anga
- ✓ Kuongeza usahihi wa utabiri wa hali ya hewa na hivyo kupongezwa na wajumbe wa Bunge la 10 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye vikao vya bajeti
- ✓ Sambamba na kupata vyeti (certificates of appreciation) kutoka Mamlaka ya Huduma za Usafiri wa Baharini Zanzabar (ZMA) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Kitengo cha Maafa kwa mchango wa TMA katika utoaji taarifa sahihi na kwa wakati kwa watumiaji wa bahari vilevile kuweshwa serikali kubabiliana na majanga yatokanayo na hali mbaya ya hewa.

Aidha katika uteuzi wake kama mjumbe wa kamati kuu ya WMO, Dkt. Kijazi aliteuliwa katika vikosi kazi viwili vya kukabiliana na majanga na usawa na jinsia (WMO EC Working Groups namely WMO-EC Advisory Panel on Disaster Risk Reduction and WMO-EC Working Group on Gender).

Kamati Kuu ya WMO inajumuisha wajumbe 37 kutoka taasisi za hali ya hewa Duniani ambao hufanya kazi kwa manufaa ya nchi mwanachama wa WMO na hukutana kila mwaka mara moja kufanikisha utekelezaji wa makubaliano ya mkutano mkuu unaofanyika kila baada ya miaka 4.

